**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**650** **HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2022**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org

TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza kwa ufupi tofauti ya dhana ya:

   (a) Kanuni na sheria

   (b) Mpira wa kikapu na mpira wa pete katika muktadha wa somo la Haiba na Michezo.
2. Fafanua stadi nne za msingi ambazo mwanafunzi lazima awe nazo ili kumwezesha kucheza mpira wa miguu kwa ufanisi.
3. Fafanua kwa kifupi zana nne zinazoweza kutumika katika kupima maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma na kitabia.
4. Bainisha sifa nne za kitabu cha kiada.
5. Taje makundi manne ya zana za kufundishia na kujifunzia na namna anavyoweza kutumia katika ufundishaji wake.
6. Eleza mbinu nne mbadala za upatikanaji wa zana za kufundishia na kujifunzia.
7. Bainisha mada nne na kueleza jinsi atakavyofundisha kila mada kwa kuzingatia misingi ya ufundishaji.
8. Eleza matumizi ya nyaraka nne zinazotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.
9. Changanua vipengele vinne vya kimaudhui vilivyopo kwenye muhtasari wa somo la Haiba na Michezo atakavyosisitiza pindi anamkabidhi somo mwalimu mwingine kwa ajili ya kufundisha.
10. Eleza umuhimu wa kufanya upimaji wa somo la Haiba na Michezo kwa wanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo.

**SEHEMU B (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Tumia hoja tano kueleza changamoto zinazoweza kujitokeza ikiwa sheria na kanuni katika michezo hazitazingatiwa.
12. Kanusha kauli "Ushiriki wa wanafunzi katika michezo hauna tija yoyote katika maisha yao" kwa kutumia hoja tano.
13. Toa hoja tano kueleza umuhimu wa Azimio la Kazi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Haiba na Michezo.
14. Shauri mambo matano anayopaswa kuzingatia mwalimu wakati wa usahihishaji wa kazi za wanafunzi katika somo la Haiba na Michezo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org